

# Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Tanzania



## Mafunzo Yaliyotokana na Mchakato wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA)

Paschal Assey, Stephen Bass, Blandina Cheche, David Howlett, George Jambiya, Idris Kikula, Servacius Likwelile, Amon Manyama, Eric Mugurusi, Ruzika Muheto na Longinus Rutasitara

# Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Tanzania

## Mafunzo Yaliyotokana na Mchakato wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA)

Paschal Assey, Stephen Bass, Blandina Cheche, David Howlett, George Jambiya, Idris Kikula, Servacius Likwelile, Amon Manyama, Eric Mugurusi, Ruzika Muheto na Longinus Rutasitara

**Nukuu:** *Assey na wenzake* 2007. Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Katika Tanzania; *Mafunzo yaliyotokana na Mchakato wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA)*. Toleo la Maliasili Na. 6. Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo. IIED, London, Uingereza.

Kimetafsiriwa na Ofisi ya Makamu wa Rais 2008

**Nakala za Kiingereza za kitabu hiki zinapatikana:**
Earthprint, P.O. Box 110, Stevenage, Hertfordshire, SG1 4TP, UK.
Barua pepe: iied@earthprint.com
Tovuti: www.earthprint.com; www.iied.org
Simu: +44 (0)1438 748111
Nukushi: +44 (0) 1438 748844

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**
Stephen Bass, Kikundi cha Maliasili
International Institute for Environment and Development (IIED)
3 Endsleigh Street, London, WC1H 0DD, UK
Simu: +44 (0)20 7388 2117
Nukushi: +44 (0) 207 388 2826
Barua pepe: Stephen.bass@iied.org

**Matoleo ya maliasili**
Lengo kuu la matoleo ya maliasili ni kuonyesha umuhimu wa mabadiliko ya kisera, kitaasisi na masoko yanayopaswa kufanyika ili maliasili itumike kwa njia endelevu ili kuondoa umaskini.

Ripoti mbalimbali za maliasili kwa lugha ya kiingereza zinapatikana katika taasisi ya IIED katika tovuti yao yenye anuani www.iied.org

Usanifu ulifanywa na Eileen Higgins, anuani pepe: eileen@eh-design.co.uk
Picha zote zilitayarishwa na Judy Rogers

ISBN: 978-1-84369-723-7
ISSN: 1605-1017

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Dibaji | ii |
| Utangulizi | iv |
| Vifupisho | v |
| 1. Mchakato wa kujumuisha mazingira na maendeleo | 1 |
| 2. Mabadiliko ya uelewa na utambuzi kuwa mazingira ni msingi wa maendeleo | 3 |
| 3. Kipindi cha mpito – michakato ya maandalizi ya sera na mipango kujumuishwa | 7 |
| 4. Mabadiliko katika mfumo wa misaada – Tanzania kuongoza maamuzi ya misaada ya maendeleo | 15 |
| 5. Mbinu zinazofaa katika harakati za kujumuisha masuala ya mazingira | 17 |
| 6. Tathmini ya matokeo ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira mpaka sasa | 23 |
| 7. Changamoto za Utekelezaji | 27 |
| 8. Uzoefu uliotokana na ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika MKUKUTA | 31 |
| Rejea | 35 |

# Dibaji

Siku hizi uhusiano wa umaskini na uharibifu wa mazingira unaeleweka vizuri. Mathalani, uharibifu wa mazingira husababisha umaskini kwa kupunguza upatikanaji wa maji safi, rutuba katika udongo, mazao na huduma nyingine muhimu kwa afya na maisha ya binadamu. Aidha umaskini nao husababisha uharibifu wa mazingira kwa kudhoofisha juhudi na uwezo wa binadamu kusimamia na kutumia rasilimali kwa njia endelevu.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao ni mwongozo muhimu katika kuleta maendeleo endelevu, unatambua kuwa mazingira bora ni msingi wa maendeleo endelevu na kupunguza umaskini. Mkakati huu umeainisha malengo kumi na tano (15) yanayohusu mazingira. Utekelezaji wa MKUKUTA unahusisha wadau mbalimbali. Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR) inalo jukumu la kuratibu ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango na bajeti za kisekta za kupunguza umaskini. Katika kutekeleza jukumu hili, OMR imefanikisha na inaendelea kutekeleza mipango na programu kadhaa ikiwemo ile ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Mazingira na Kanuni zake.




Sera ya Taifa ya Mazingira ya 1997 imeainisha changamoto sita ambazo ni: uharibifu wa ardhi; uharibifu wa misitu; kupotea kwa makazi ya viumbe-pori na bioanuai; kukosekana kwa maji salama mjini na vijijini; kupungua kwa ubora wa mifumo ya maji; na uchafuzi wa mazingira hasa katika maeneo ya mijini. Changamoto hizi zinachangia kuzorotesha ukuaji wa uchumi na juhudi za serikali katika kupunguza umaskini, na hivyo kuathiri maisha na ustawi wa jamii.

Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 imeeleza wazi wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali kuanzia serikali za mitaa hadi taifa. Mambo yanayosisitizwa katika Sheria hii ni mipango na usimamizi wa matumizi endelevu ya mazingira: kudhibiti uchafuzi wa mazingira; utunzaji wa taarifa na takwimu za mazingira; utafiti na ushiriki wa jamii, utekelezaji wa majukumu yatokanayo na mikataba ya kimataifa, utii na utekelezaji wa sheria pamoja na matumizi ya dhana mbalimbali za kusimamia hifadhi ya mazingira hususani Tathimini ya Athari katika Mazingira (TAM); Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK), dhana za kiuchumi na viwango vya mazingira. Aidha kanuni, miongozo na programu mbalimbali zimetungwa ili kufanikisha utekelezaji wa sheria hiyo.

OMR imefanya tathmini kuhusu uwezo wa wadau kusimamia utekelezaji wa Sheria ya mazingira kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa na kuandaa programu ya utekelezaji ambayo inazingatia kuimarisha mfumo wa uwezeshaji. Pia OMR ilisimamia utayarishaji wa viashiria vya kufuatilia kupungua kwa umaskini na kuboresha mazingira vitakavyotumika kupima mwenendo na uwiano baina ya umaskini na mazingira. Mfumo huu umeweka misingi ya kuelekeza mchakato mzima wa kujumuisha masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo katika Tanzania.

Katika kitabu hiki, waandishi wanachambua mafanikio yaliyopatikana wakati wa kuandaa MKUKUTA, namna yalivyopatikana na kuainisha changamoto zilizoko mbele yetu.



**Abubakar R. M. S. Rajabu**
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais

# Utangulizi

Kitabu hiki kimetafsiriwa na kikundi cha wachambuzi wakiwemo wafanyakazi wa Serikali na wasio wa Serikali kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Uchapishaji wa kitabu hiki umefadhiliwa na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo [*International Institute for Environment and Development (IIED)*] kufuatia mafanikio ya Tanzania katika kujumuisha masuala ya Mazingira katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Lengo la chapisho hili ni kuweka kumbukumbu kuhusu tuliyojifunza wakati wa kujumuisha masuala ya mazingira katika sera na mipango ya maendeleo kwa kuweka bayana mafanikio na changamoto. Hata hivyo uzoefu umeonyesha kuwa MKUKUTA ni mkakati wenye taswira ya mfano wa kukubalika na kwamba sera zilizotengenezwa na serikali zinazingatia kanuni za Mkakati wa Benki ya Dunia wa Kupunguza Umaskini.

Matarajio ni kuwa kitabu hiki kitatoa mafunzo juu ya umuhimu wa kujumuisha masuala ya mazingira katika mipango ya kuondoa umaskini Tanzania na nchi nyingine. Kwa kupitia chapisho hili tunategemea kubadilishana uzoefu kati ya wadau mbalimbali wanaoshughulika na masuala ya kujumuisha mazingira katika mipango ya maendeleo. Tuliyojifunza ni mengi na tungependa kusisitiza dhana ya kubadilishana uzoefu katika ngazi zote ndani na nje ya nchi.



## Tafsiri ya kitabu hiki

Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na mashirika mbalimbali ya Kimataifa hasa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) kwa kufadhili awamu ya pili ya Mradi wa kujumuisha mazingira katika Utekelezaji wa MKUKUTA. Aidha, tunatoa shukrani kwa Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED) waliogharamia uchapishaji. Shukrani za pekee ziwaendee Godlove John Mwamsojo na Julius Shilungushela kwa kufanya tafsiri ya kwanza.

Tunapenda ieleweke kwamba,watafsiri wanahusika na usahihi au mapungufu yoyote yaliyomo katika kitabu hiki.

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| OMR | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| TMK | Tathimini ya Mazingira Kimkakati |
| MKU | Mkakati wa Kupunguza Umaskini |
| AZISE | Asasi Zisizo za Serikali |
| TAM | Tathimini ya Athari katika Mazingira |

# Mchakato wa kujumuisha mazingira na maendeleo

Kitabu hiki kimeandaliwa ili kueleza mafanikio na changamoto zilizotokana na mchakato wa muda mrefu wa kujumuisha masuala ya Mazingira katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Hasa mabadiliko katika maeneo muhimu matatu yafuatayo.

*Kukua kwa ufahamu kuhusu Mazingira*
Hapo awali suala la mazingira halikupewa kipaumbele katika mipango ya maendeleo ya uchumi na kuondoa umaskini. Hivi sasa uelewa wa jamii umeongezeka na masuala ya mazingira yanapewa kipaumbele katika kuandaa mipango ya maendeleo. Hii inatokana na ukweli kuwa matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira mijini na vijijini yamekuwa bayana. Hali hii imetambuliwa na uongozi wa nchi, hususan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Jakaya Mrisho Kikwete ambaye amefanya suala la mazingira kuwa miongoni mwa mambo kumi muhimu ya kushughulikiwa na serikali. Mchakato wa kujumuisha mazingira katika MKUKUTA ulihusisha ukusanyaji wa maoni, mawazo, mifano na kuwakutanisha viongozi mbalimbali, hali iliyosaidia kukua kwa ufahamu miongoni mwa watoa maamuzi pia (angalia sura ya 2).

*Mchakato wa Uandaaji wa Mipango na Mikakati*
Mikakati ya maendeleo ya hapo awali ilitoa kipaumbele kwa sekta chache bila kuhusisha mazingira na masuala mengine mtambuka na wadau wake. Sasa hivi utaratibu wa kitaifa wa kuandaa mipango ni wa ushirikishwaji na hivyo huzingatia matakwa ya wadau. Mchakato wa MKUKUTA umesaidia kuboresha uhusiano na taratibu za kuandaa mipango katika nyanja za umaskini, usimamizi wa fedha na sheria ya mazingira (angalia sura 3).

*Ubia na wafadhili*
Hapo awali, mipango ya maendeleo iliendana na masharti ya wafadhili. Hivi sasa hali hii imebadilika. Serikali ndiyo inayotoa mwongozo na wafadhili huelekeza misaada yao kulingana na malengo ya serikali. Mchakato wa MKUKUTA unatoa fursa kwa wadau kuamua njia nzuri ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango na shughuli zao.

Katika kuratibu ujumuishaji wa mazingira, OMR ilizingatia ushirikishaji wa wadau wanaoathirika na mabadiliko; utambuzi wa mambo mapya na uhamasishaji wa mabadiliko. Dhana na mbinu nyingine zilizotumiwa zimeelezwa zaidi katika sura ya 5.

Hata hivyo, ujumuishaji wa mazingira katika MKUKUTA hautakamilika hadi hapo masuala ya usimamizi wa mazingira yatakapozingatiwa katika bajeti, miradi ya uwekezaji na utawala bora. Mpaka sasa kuna baadhi ya changamoto zinaonekana kupatiwa ufumbuzi kwa mfano.

- Ufinyu wa bajeti – Ili kuondoa umaskini na kuboresha maisha, serikali kupitia Wizara ya Fedha imeongeza bajeti ya utekelezaji wa majumuisho ya mazingira mara tano zaidi katika bajeti ya mwaka 2006/07 ikilinganishwa na ile ya 2005/06.



**Mabadiliko ya Tabia Nchi Yanaendelea Kujidhihirisha hapa Tanzania**

- Uwezo mdogo wa kusimamia mazingira – Ili kuongeza uwezo wa kusimamia mazingira, upatikanaji wa taarifa za mazingira ni muhimu. Hivyo serikali imebainisha majukumu ya mamlaka mbali mbali za usimamizi wa mazingira ikiwemo Idara ya Mazingira, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na wadau wengine.

- Ugatuzi wa madaraka kwa wadau wa mazingira – Mchakato wa MKUKUTA ulikuwa shirikishi ili maskini waweze kufahamu haki na majukumu yao, fursa zilizopo katika kutumia raslimali na kuondoa tofauti baina ya matabaka mbalimbali ya kijamii Changamoto ni jinsi ya kuhakikisha kuwa juhudi hizo zinadumu katika utekelezaji wa MKUKUTA.



**Sanduku Na.1.** Dondoo Kuhusu MKUKUTA

- Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) uliidhinishwa na Baraza la Mawaziri Februari 2005, kwa utelezaji katika kipindi cha miaka mitano.
- Ni muendelezo wa Waraka wa Mkakati wa kupunguza Umaskini wa mwaka 2000.
- Unatokana na Dira ya Taifa kufikia mwaka 2025 (iliyoweka malengo ya maendeleo ya muda mrefu) na malengo ya kimataifa ya changamoto ya milenia.
- Ushirikishwaji wa wadau na umiliki wa mkakati kitaifa ni mambo ya msingi yaliyozingatiwa wakati wa maandalizi yake. Mambo haya yanaendelezwa katika utekelezaji na maandalizi ya sera mbalimbali na hivyo kuendelea kujumuisha matakwa ya wadau.
- MKUKUTA unalenga matokeo na unasistiza uboreshaji wa ushirikiano baina ya sekta na wadau wote watakaosaidia kufikia matokeo hayo.
- Matokeo tarajiwa makuu ni kukua kwa uchumi na utawala bora. Msisitizo umewekwa katika maboresho ya sheria na kuondoa desturi zinazokwamisha ukuaji wa uchumi na kuathiri makundi ya jamii.
- Mkakati unahitaji nyezo na fedha na hivyo umeunganishwa na bajeti ya serikali na Mkakati wa pamoja wa kuchangia maendeleo baina ya Serikali na Wafadhili.
- MKUKUTA umejumuisha masuala mtambuka yakiwemo masuala ya jinsia, UKIMWI, Ulemavu, watoto,wazee, ajira, makazi na mazingira.

# Mabadiliko ya uelewa na utambuzi kuwa mazingira ni msingi wa maendeleo

> *Umaskini na uharibifu wa mazingira ni watoto mapacha na mama yao ni ujinga* Mhe. (Ali Hassan Mwinyi 1998)

Ni siku za karibuni tu, mtazamo wa muda mrefu, kwamba suala la mazingira ni jambo la kuchelewesha maendeleo umeanza kubadilika. Hii inatokana na ukweli kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa dhahiri na kuathiri maisha ya wananchi hasa wale maskini zaidi. Mabadiliko haya yamesaidia kuongeza hali ya usikivu na tahadhari miongoni mwa wanasiasa juu ya umuhimu wa mazingira bora kwa maisha ya watu, afya, kukua kwa uchumi na usalama.

Sera ya Mazingira ya mwaka 1997 imeainisha matatizo makuu sita ya mazingira yanayoikabili nchi yetu. Matatizo haya ni:

- Uharibifu wa ardhi
- Kutopatikana kwa maji safi kwa wakazi wa mjini na vijijini;
- Uchafuzi wa mazingira
- Upotevu wa makazi ya viumbe – pori na bioanuai
- Uharibifu wa makazi ya viumbe wa majini; na
- Uharibifu wa misitu



**Athari za Uharibifu wa Mazingira Kama Vile Mafuriko Zitaongezeka Kutokana na Mabadiliko ya Tabia Nchi**

Pamoja na kuainisha matatizo haya katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, bado hali ya mazingira haijawa nzuri katika maeneo yafuatayo: mafuriko na ufyekaji wa misitu; mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla hasa maeneo yaliyokaliwa na wakimbizi. Hali hii imechangia kuathiri ustawi wa jamii na maendeleo kwa ujumla.

## Taarifa za kitaalamu kuhusu mahusiano baina ya mazingira na umaskini

Watanzania wengi sasa hivi wanaelewa kuwa uchumi wa nchi na maisha yanategemea sana mazingira bora. Uchunguzi uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Masuala ya Jamii (ESRF) mwaka 2003 umebainisha kuwa mambo makuu yanayosababisha umaskini ni uchumi duni, uharibifu wa mazingira na kukosekana

kwa utawala bora. Ukweli huu umedhihirika katika taarifa ya uhakiki wa matumizi ya umma kuhusu mazingira na ile ya uchunguzi wa Benki ya Dunia kuhusu hali ya uchumi wa Tanzania kama ifuatavyo:

- Mazingira kama rasilimali
  Takribani asilimia 76 ya wananchi vijijini wanategemea maliasili kwa maisha yao na asilimia 95 ya nishati hutokana na kuni huku rutuba katika udongo ikizidi kupungua, misitu na maji safi na salama vikipotea. Aidha asilimia 47 ya wananchi vijijini hutumia maji yasiyo salama ambayo huyafuata mbali na makazi yao.

- Usalama wa mazingira na uendelevu wa sekta kuu za uchumi.
  Asilimia 45 ya mapato ya ndani ya nchi na asilimia 60 ya mapato ya soko la nje hutegemea kilimo. Kwa wakati huu tunaweza pia kuongeza sekta ya madini ambayo inakuwa kwa asilimia 17 pamoja na sekta za Utalii na Uvuvi zinazokua kwa asilimia 7 kwa mwaka. Sekta hizi zote zinatishiwa na uharibifu wa mazingira.




**Upatikanaji wa maji ni suala la Umaskini na pia la Mazingira**

Tafiti zimeonyesha kuwa kiasi cha dola za Marekani bilioni moja zinapotea kila mwaka kutokana na kupungua kwa mazao ya misitu, uvuvi na wanyama pori. Pia inaonesha kuwa ukame wa mwaka 2003 ulisababisha kupungua kwa kiwango cha kukua kwa uchumi kwa asilimia 10. Matokeo ya tafiti hizo yanaashiria kuwa matatizo yatakuwa makubwa zaidi katika siku za baadaye endapo uharibifu wa mazingira hautapatiwa ufumbuzi hasa ukizingatia mabadiliko ya tabianchi kama vile maafa yaliyotokana na mafuriko yaliyotokea wakati wa El Niño na kuzama kwa kisiwa cha Maziwe ambacho kilikuwa mazalia ya kasa na samaki katika pwani ya Pangani mkoani Tanga. Kufikia hatua hii, watetezi wa mazingira wamefanya kazi ya kutosha, na taarifa zote hizi zitakuwa kazi bure kama hazitapewa kipaumbele na wanasiasa.

## Mchango wa wanaharakati wa mazingira katika kukuza uelewa na kuleta mabadiliko ya kisiasa

Wanaharakati wa Mazingira wa ndani na nje ya nchi wanafanya kazi kubwa kubadilisha mtazamo wa wanasiasa na jamii kuhusu masuala ya mazingira. Sasa hivi mazingira yamepewa kipaumbele katika mipango ya serikali. Kwa mfano,

suala la upatikanaji wa maji limeingizwa katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, na pia katika MKUKUTA. Hali hii imewatia ari wanaharakati na kuongeza heshima ya vikundi vya jamii na wataalamu wa mazingira. Pia imesaidia kuongezeka motisha na uhalali wa watumishi wa serikali kujihusisha kwa umakini zaidi na masuala ya mazingira.



**Kampeni ya Vyombo vya Habari Imesaidia Kufichua Biashara Haramu ya Magogo**

## Vichocheo vingine vya kukua kwa uelewa

*Ushiriki wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa za Mazingira* – Ongezeko la makala za mazingira kupitia vyombo vya habari linaashiria kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya mazingira miongoni mwa wanahabari. Mfano mzuri ni jinsi vyombo vya habari vilivyosaidia kueneza taarifa kuhusu madhara ambayo yangesababishwa na mradi wa ufugaji kamba katika delta ya Mto Rufiji ambao ulipendekezwa na kampuni ya African Fishing mnamo mwaka 1995. Kampuni hii ilikusudia kuhamisha watu kutoka katika makazi yao na kuchukua maeneo ya kilimo cha mpunga. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilisimamia na kufanya mapitio ya TAM na mashauriano na wadau wote na kuthibitika kwamba mradi ungekuwa na madhara makubwa ambayo yangesababisha njaa, uchafuzi wa ardhi na maji, kuathiri shughuli za uvuvi na kuongezeka kwa umaskini. Mfano huu unadhihirisha kwamba TAM ni dhana muhimu katika kuhifadhi mazingira na kulinda maslahi ya jamii.

Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 inatamka kuwa TAM ni suala la kisheria katika Tanzania, na kwa kuwa mchakato wa TAM ni shirikishi, vyombo vya habari vimeshiriki kufafanua athari zinazoweza kusababishwa na baadhi ya miradi kwa maisha ya jamii. Pia vimesaidia kutangaza umuhimu wa kufanya TAM na ushiriki wa jamii. Aidha kuongezeka kwa miradi inayofanyiwa TAM ni dalili ya kukua kwa mwamko kuhusu mazingira kwa watoa maamuzi, wawekezaji na wafadhili.

Mfano mwingine ni namna vyombo vya habari vilivyosaidia kueleza madhara ya uvunaji wa miti kwa ajili ya magogo ulivyokuwa umekithiri katika mikoa ya Lindi na Pwani. Makala zilionyesha jinsi shughuli hiyo inavyoweza kusababisha umaskini kwa jamii inayotegemea mazao ya misitu. Taarifa hizi zilisaidia kuchochea ari ya wananchi kudai TAM ifanyike kwa kila shughuli ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

**Sanduku Na. 2.** Mradi wa ufugaji kamba katika bonde la mto Rufiji na Tathmini ya Athari katika Mazingira (TAM)

Mnamo mwaka 1995 mradi mkubwa wa kufuga kamba katika bonde la Mto Rufiji ulipendekezwa. Utekelezaji wa mradi huu ungeleta athari kubwa kwa jamii inayoishi katika bonde hilo. Athari hizo ni pamoja na kuwahamisha watu kutoka katika makazi yao, kupungua kwa eneo kwa ajili ya shughuli za kilimo jambo ambalo hatimaye lingeweza kusababisha njaa,Uharibifu wa ardhi, uchafuzi wa maji, uharibifu wa mazalia ya viumbe wa baharini na kuathiri shughuli za uvuvi katika eneo hilo. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilifanya TAM na kubaini athari za mradi huo katika mazingira na jamii. TAM ilihusisha mashauriano na wadau, na kuthibitika kwamba mradi ungekuwa na madhara makubwa ambayo yangesababisha umasikini kwa watu. Serikali ilipendekeza njia mbalimbali za kukabiliana na madhara, hayo ambayo haikuwa rahisi kwa wawekezaji kutekeleza, hivyo utekelezaji wa mradi huu ulisitishwa. Kwa jinsi hii tumeweza kuona kuwa TAM ni dhana muhimu katika kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali, kutunza mazingira na kulinda maslahi ya jamii.

*Taarifa za progamu zinazohusu masuala ya umaskini na mazingira*, Programu mbalimbali zilizotekelezwa zimekuwa kielelezo kwa wadau jinsi ya kujumuisha mazingira katika MKUKUTA kwa ukamilifu zaidi. Haya yalitokana na mashauriano ya ndani ya serikali na vyama visivyo vya kiserikali. Kwa mfano Mradi wa Mazingira wa Ziwa Victoria ulielezea kwa uwazi matatizo ya uchafuzi wa mazingira utokanao na majitaka kutoka viwandani na majumbani pamoja na magugu maji yanavyosababisha madhara kwa maisha ya watu wapatao milioni tatu.



*Maboresho na uwezeshaji wa serikali za mitaa* – Mfumo wa utayarishaji wa mipango kwa kuzingatia Fursa na Vikwazo (F&K) na kwa kutumia kamati za mazingira umetoa nafasi kwa jamii kuainisha umuhimu wa masuala ya mazingira na umaskini na kuyajumuisha katika mipango ya maendeleo ya serikali za mitaa.

*Changamoto katika utendaji wa taasisi za umma* – Utendaji wa taasisi za umma zinazosimamia maliasili umekuwa ukizorota na kusababisha madhara kwa jamii. Wakati huohuo mifumo shirikishi ya usimamizi wa maliasili haijapanuliwa na kuonekana kama kikwazo kinachozuia umma kuzalisha mazao yatokanayo na mazingira. Kwa mfano Mpango Shirikishi wa Usimamizi wa Misitu unatumika katika Asilimia moja tu ya misitu ya hifadhi na Mpango Shirikishi wa Usimamizi wa Wanyamapori bado uko katika majaribio. Kwa kuwa ahadi za kuboresha maisha na hifadhi ya mazingira zilizokuwa zinatolewa wakati wa kuandaa mipango hii hazijatekelezwa, wadau wengi wametoa ushauri kwamba mazingira yapewe kipaumbele katika MKUKUTA.

*Kuimarika kwa shughuli za mazingira katika asasi za kijamii* – Uzoefu unaonesha kuwa shughuli za asasi nyingi za jamii zilihusu maendeleo ya kiuchumi na huduma za jamii. Hivi sasa asasi nyingi zimepanua wigo wa majukumu yao na kushughulikia suala la mazingira na umaskini. Pia taasisi za kimataifa zisizokuwa za kiserikali kama WWF na IUCN zilishughulikia masuala ya hifadhi ya mazingira pekee, lakini sasa zimeanza kushughulikia pia masuala ya kuondoa umaskini.

3

# Kipindi cha mpito – michakato ya maandalizi ya sera na mipango kujumuishwa

Mchakato wa MKUKUTA ulitumia uzoefu wa nchi katika kuandaa sera na mipango ya kuondoa umaskini na usimamizi wa mazingira ili kuthibitisha kuwa masuala haya yana muingiliano. Mchakato huu umedhihirisha umahiri wa wataalam wa kuandaa mipango ambayo ni dalili za kufikiwa kwa malengo ya Mwalimu J.K.Nyerere ya sera ya Ujamaa na Kujitegemea.

## Mapitio ya mipango ya maendeleo kabla ya MKUKUTA

Ili kuuelewa masuala yaliyoibuliwa na MKUKUTA kuna umuhimu wa kuangalia mikakati mikubwa mitatu ya maendeleo iliyotangulia ambayo ni: Dira ya Maendeleo hadi mwaka 2025 (1996); Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini wa mwaka 1997 na ule wa mwaka 2000. Mikakati hii na jitihada nyingine za maendeleo na kuboresha mazingira pia zinaonyeshwa katika jedwali na 1.

*Dira ya maendeleo 2025* – Dira hii inatoa mwelekeo na matokeo tarajiwa ya mipango ya maendeleo yatakayoleta maisha bora, amani, umoja, utengemano na kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025. Dira inasisitiza uandaaji shirikishi wa mipango na inatambua umuhimu wa mazingira na maendeleo endelevu.

*Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini (1997)* – Huu ulikuwa mkakati wa kwanza ulioandaliwa kwa lengo la kuondoa umaskini ukiwa na madhumuni ya kukuza uchumi na kuongeza ajira kupitia sekta za kilimo, viwanda, nyumba na maji. Aidha mkakati huu ulitambua kuwa mazingira ni suala mtambuka na ulizingatia kanuni ya kujifunza kutokana na matokeo. Mkakati huu haukupata wafadhili kutokana na Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha Duniani kutoridhika na maandalizi yake. Kwa msukumo wa wafadhili Tanzania iliandaa Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa 2000.

*Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (2000)* – Waraka huu uliandaliwa kwa msukumo wa Benki ya Dunia likiwa ni sharti la kupunguziwa madeni japo ulikuwa na sura ya kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Umaskini (1997). Mkakati huu ulibadilisha mwelekeo na kuwa na malengo ya huduma za kijamii badala ya kukuza uchumi na ulilenga katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Barabara, Mahakama, na baadhi ya vipengele vya Kilimo), pamoja na Virusi Vya Ukimwi/Ukimwi na masuala mengine mtambuka pamoja na sekta ya ardhi iliyoongezwa baadaye. Waraka huu uliandaliwa kwa kushirikisha wadau wachache na hivyo kukosa malengo mahususi tofauti na mkakati wa kwanza. Hii ilitokana na kutoshirikisha mamlaka na vyama vinazosimamia mazingira. Hivyo maandalizi ya waraka huu yalionekana kama kurudi hatua moja nyuma.

**Jedwali Na. 1.** Mfululizo wa jitihada za ujumuishaji wa mazingira katika harakati za kupunguza umasikini

| Mwaka | Mazingira | ⇦Wahusika Wakuu/kisababishi⇨ | Kupunguza Umasikini |
|---|---|---|---|
| 1994 | Mpango wa utekelezaji wa Mazingira | ⇦Benki ya Dunia | |
| 1995 | Ilani ya Mazingira; Mkutano wa Taifa wa Umaskini na Mazingira | ⇦ Wanaharakati wa mazingira nchini<br>⇦ Kujiri kwa uchaguzi mkuu ulioshirikisha vyama vingi | |
| 1996 | Idara ya Mazingira pamoja na Umaskini kuwekwa Chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais | ⇦Viongozi wa Kitaifa | Dira ya Maendeleo – 2025 (ilichapishwa 1999) |
| 1997 | Kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira | ⇦Wanaharakati wa Mazingira<br>Wanaharakati wa Maendeleo⇨ | Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini (kufuatia Dira 2025) |
| 2000 | Marekebisho ya muundo wa Kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa Mazingira | ⇦Benki ya Dunia⇨ | Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini 2000/3 |
| 2001 | Mashauriano na maandalizi ya programu ya ujumuishaji wa suala la mazingira | ⇦Ofisi ya Makamu wa Rais⇨<br>Benki ya Dunia, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP)⇨ | Mfumo wa ufuatiliaji wa kupunguza Umaskini, Mkakati wa Misaada |
| 2002 | Utekelezaji wa programu ya ujumuishaji wa suala la mazingira unaanza | | |
| 2003 | | Vyama visivyo vya kiserikali (NGOs)⇨ | Mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini |
| 2004 | Uhakiki wa matumizi ya umma katika sekta ya mazingira; Ufuatiliaji wa masuala ya kupunguza umaskini na viashiria vya mazingira | ⇦Wizara ya Fedha⇨<br>⇦Viongozi wa Kitaifa⇨<br>⇦Ofisi ya Makamu wa Rais/ ⇨<br>Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa | |
| 2004 | Kutungwa kwa Sheria ya Mazingira ya 2004; | ⇦Benki ya Dunia⇨<br>⇦Vikundi vya Kijamii⇨<br>⇦Wafadhili⇨ | MKUKUTA 2005-9 |
| 2006 | Taarifa ya kitaifa kuhusu hali ya Mazingira | ⇦Wafadhili⇨<br>⇦Ofisi ya Makamu wa Rais⇨ | Bajeti ya Kupunguza Umaskini – Mkopo 2006-10 |

## MKUKUTA (2005): Mkakati unaozingatia matokeo katika kupanga

Maandalizi ya MKUKUTA yamezingatia matakwa ya walengwa na hivyo kuongeza umiliki wa wadau katika mipango ya maendeleo. Hali hii ni tofauti na mipango ya awali ambayo haikuzingatia ushirikishwaji wa wadau na iliandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya wafadhili na maelekezo kutoka kwenye mamlaka za juu. Mafanikio ya mchakato wa maandalizi ya MKUKUTA yametokana na mambo yafuatayo:

*MKUKUTA ulisimamiwa na uongozi wa juu kisiasa* – Maandalizi ya MKUKUTA yalipata msukumo wa viongozi wa juu wa serikali akiwemo Rais mwenyewe aliyekuwa tayari kutoa ushauri wakati wote wa maandalizi. Hii iliongeza ari na hamasa kwa wataalam, kuimarisha mashauriano na jamii na mijadala katika sekta mbalimbali. Ushirikishwaji wa bunge na wanasiasa wengine katika mchakato wa uandaaji wa MKUKUTA uliongeza uelewa na umiliki wa MKUKUTA.

Mchakato huu ulioratibiwa na OMR ulisaidia kujumuisha masuala ya sekta mbalimbali na hasa Umaskini na Mazingira ambayo yote yalikuwa chini ya Ofisi hii. Ikumbukwe kwamba OMR iliratibu na kuwezesha sekta nyingine kufanya maamuzi kwa kutoa maelekezo jinsi ya kujumuisha masuala ya MKUKUTA katika sekta zao.

*Wajumbe wa Kamati ya Ufundi na Sekretariati ya MKUKUTA walitoka sekta mbalimbali* – Kamati hii ilishawishi na kuhamasisha umuhimu wa uchambuzi wa masuala mtambuka kama vile mazingira na kutoa mapendekezo.



*Mipango shirikishi inayozingatia kanuni na matakwa ya nchi* – Katika mchakato wa MKUKUTA jitihada zilifanyika kuhakikisha kwamba kanuni hizi zinafuatwa. Maandalizi shirikishi ya mipango ya nchi inayozingatia kanuni na matakwa ya wadau hudhihirisha umiliki wa kitaifa; msimamo wa kisiasa na utekelezaji wa demokrasia na haki za binadamu. Hii huwezesha kushirikisha wadau wengi



**Ni muhimu wafadhili na serikali kufanya kazi kwa pamoja kusaidia ujumuishwaji wa masuala ya mazingira katika mipango na mikakati ya maendeleo**

zaidi katika kuteua vipaumbele, matumizi ya rasilimali na ugawanaji wa faida ili kuimarisha mahusiano na kuleta maendeleo endelevu. Aidha ubadilishanaji wa uzoefu na nchi jirani ulisaidia kuboresha mchakato wa MKUKUTA.

*Matumizi ya dhana za ushirikishwaji, upembuzi na utoaji maamuzi* – Ili kupata uzoefu wa sekta mbalimbali, ushirikishwaji wa wadau ulikuwa wa mafanikio kwani wengi waliwasilisha maoni na uzoefu wao.

*Masuala mtambuka yalikuwa kitovu dhahiri cha mapitio ya waraka wa mkakati wa kupunguza umaskini* – OMR iliunda kikundi cha ushauri wa masuala mtambuka, ili kurahisisha upatikanaji wa maoni na kuwezesha vikundi kufanya kazi pamoja. Timu iliyoandaa MKUKUTA ilikuwa na wadau wenye utaalamu, upeo na uzoefu, wengi wao wakiwa ni Watanzania (wasomi, watafiti, vyama visivyo vya kiserikali na sekta binafsi) chini ya uenyekiti wa OMR. Timu hii ilikuwa makini na yenye ushawishi mkubwa na ilichambua masuala yote kwa usawa.

*MKUKUTA uligawanywa katika maeneo matatu ili kurahisisha maandalizi ya bajeti na mipango* – Maeneo haya ni maendeleo na kupunguza umaskini; maisha bora na ustawi wa jamii, na Utawala bora na uwajibikaji. Kila eneo lilinyambuliwa ili kuweka mipaka, malengo, majukumu, matokeo, watendaji, na viashiria. Mgawanyo huu wa majukumu uliwezesha kuleta ufanisi zaidi tofauti na Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Kutokana na ufanisi huu:



- *MKUKUTA umeanzisha ajenda yenye nguvu inayojitegemea, kwa mtazamo wa dira ya taifa – 2025.* Madhumuni ya muda mrefu ni kupunguza kutegemea misaada kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu na kukua kwa uchumi kwa kiwango cha 6% – 8% kwa mwaka hadi kufikia 2015 na kusisitiza usawa na utawala bora.

- *MKUKUTA unatumika kupata mwafaka wa kisiasa kuhusu umaskini* – Wahusika sio wizara za serikali pekee, bali pia serikali za mitaa, jamii na vyama vyao, sekta binafsi na wafadhili. Kuhusika kwao wakati wa kuandaa MKUKUTA kunarahisisha utekelezaji.

- *MKUKUTA ni sehemu ya michakato ya kitaifa na uendeshaji wa serikali* – Ni kichocheo na hutegemea uhakiki wa matumizi ya umma, na mkakati wa pamoja wa misaada.

- *MKUKUTA umefanikiwa kupanua ajenda ya kupunguza umaskini kwa kutegemea malengo.* Tofauti na Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU) uliozingatia sekta saba tu, MKUKUTA umezingatia malengo, ushirikishwaji wa wadau na mahitaji. Masuala ya mazingira, haki za binadamu na utawala bora.

## Uhusiano wa MKUKUTA na utekelezaji wa sera za umaskini na mazingira

Uzoefu umeonyesha kuwa ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo huchukua muda mrefu na ni matokeo ya michakato mingi na sio zoezi la mara moja. Tofauti na nchi nyingine ambako ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo hufanyika mwishoni, mchakato wa ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika MKUKUTA ulianza mapema. Kazi ya ujumuishaji wa mazingira ilihusisha mambo makuu manne:

- Tahakiki ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini
- Tahakiki ya matumizi ya umma
- Matayarisho ya sheria ya Mazingira

Matayarisho ya mfumo wa uhakiki na ufuatiliaji wa mwenendo wa umaskini.

## Umuhimu wa Programu ya Kujumuisha Mazingira katika MKUKUTA

*OMR ikishirikiana na UNDP iliandaa na kuratibu utekelezaji wa mradi wa kujumuisha masuala ya mazingira na umaskini ambayo ilikuwa kichocheo cha kuhakikisha masuala mtambuka yanatiliwa mkazo katika* MKUKUTA.
Malengo ya programu hii ni:

- Kuongeza ufahamu jinsi masuala ya mazingira yanavyoathiri maisha ya jamii na ukuaji wa uchumi.
- Tathmini ya matumizi, mapato na mchango wa mazingira katika mipango.
- Kuandaa viashiria vya umaskini na mazingira ili vitumike katika mfumo wa ufualitiaji wa MKUKUTA.
- Kujenga uwezo katika ngazi ya Taifa na Serikali za Mitaa ili kuwezesha usimamiaji wa masuala ya umaskini na mazingira.
- Kuboresha uratibu wa kujumuisha masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo.

Kutokana na nafasi yake katika muundo wa serikali OMR ilidhihirika kuwa mahali mwafaka kwa ajili ya uratibu wa kazi ya kujumuisha masuala ya mazingira katika MKUKUTA, na kuondoa hatari ya kuliona suala la Mazingira kama kazi ya taasisi moja hali ambayo ingesababisha mazingira kutojumuishwa kikamilifu katika maazimio ya MKUKUTA. Chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, OMR iliweza kushawishi Wizara ya Fedha kuingiza suala la umaskini na mazingira kama ajenda muhimu. Utetezi wa wanaharakati wa mazingira peke yake usingeweza kuleta mafanikio haya. Ili kufanikisha kazi hii, aliajiriwa mtaalamu mshauri wa progamu hiyo ambaye alisimamia masuala ya kitalaamu kuhakikisha kwamba wadau wanapata taarifa za mazingira na kuchanganua maoni ya wadau ili mchakato wa kujumuisha mazingira upewe uzito unaostahili.

## Kuundwa kwa Kikundi cha Wataalamu wa Mazingira

Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2004 na OMR ili kuhakikisha kuwa sekta zinajumuisha masuala ya mazingira na umaskini katika upangaji na utekelezaji wa mipango yao. Kikundi hiki kilishirikisha wawakilishi kutoka katika idara zinazoshughulikia masuala ya mazingira na mashirika ya wafadhili. Kikundi hukutana mara moja kila mwezi na kubadilishana taarifa na kujadiliana namna ya kuziboresha.

## Tahakiki ya Mafanikio na Changamoto za Mkakati wa Kupunguza Umaskini

Mkakati wa Kupunguza Umaskini ulifanyiwa mapitio ya mwaka mmoja (2000 – 03) kutokana na sababu kuu nne: Kwanza kuangalia kama malengo yanakidhi matakwa ya dira ya maendeleo 2025. Pili kutoa fursa ya kujifunza makosa ya nyuma yaliyotokana na kutegemea mipango ya watu wa nje. Tatu kwa kuwa uratibu wake uko katika OMR ingewezesha kupanua mawanda ya tahakiki ili kuingiza masuala ya mazingira katika sekta. Mwisho kuonyesha njia muafaka ya kuibua majadiliano ya wadau ili kuboresha mkakati.

Ili kufanikisha mchakato wa tahakiki, OMR ilitayarisha maswali ambayo yalisambazwa kwa wadau wote. Mambo yaliyozingatiwa ni fursa zilizopo katika mazingira kwa ajili ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini, vijijini na mijini na kusisitiza haja ya kutunza mazingira ili kufikia maendeleo endelevu. Hii ilisaidia kuondokana na mtazamo wa zamani kwamba mazingira ni kikwazo cha maendeleo.



*Mafanikio:*

Uanzishaji wa tahakiki ya Matumizi ya Umma (Public Expenditure Review) imetoa nafasi nzuri kwa masuala ya mazingira kupangiwa bajeti kisekta. Mfumo huu ulibainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na vile ambavyo havihusiani na makusanyo ya kodi. Vyanzo hivi ni pamoja na vile vya mazingira na maliasili ambavyo havikuwa vinapewa kipaumbele na bajeti hapo awali. Hii ilisaidia kubadili mtazamo wa wizara ya fedha na kuifanya ione kuwa Mazingira ni kitega uchumi.

Hapo awali wizara ya fedha haikutoa kipaumbele katika bajeti kwa masuala ya mazingira ingawa uchumi wa Tanzania hutegemea maliasili. Wizara ya fedha ilikuwa inategemea kuona ongezeko la mapato yasiyotokana na kodi kutokana na maliasili na mazingira. Hivyo wizara iliomba uchunguzi ufanyike katika sekta za mazingira, nishati na ardhi wakati wa zoezi la mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini ili kuona mchango wake katika pato la Taifa.

Mkakati ulikusudia kuanzisha viwango, mwelekeo, na mgawanyo wa matumizi ya serikali katika mazingira ili kukidhi vipaumbele vya nchi kwa nia ya kupunguza umaskini. Baada ya kutumia takwimu za miaka miwili (2000/01- 2001/02), utafiti ulibainisha kuwa:

- Kuna umuhimu wa kutafakari juu ya rasilimali za mazingira na mchango wake katika pato la taifa
- Kuna bei ndogo na ukusanyaji mdogo wa maduhuri katika mazao ya maliasili; mfano katika misitu, uvuvi, na wanyama pori
- Kuna bajeti ndogo kwa wilaya
- Masuala ya mazingira kutopewa kipaumbele na hivyo bajeti ndogo kwa ajili ya shughuli za mazingira
- Baadhi ya sekta zinazotegemea maliasili kutotenga bajeti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira

Ujumuishaji wa masuala ya mazingira haukuwa katika utaratibu wa serikali wa upangaji wa bajeti.

Hatimaye ujumuishaji wa mazingira katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini umependekeza ongezeko la matumizi ya mazingira hasa katika serikali za mitaa zinazosimamia moja kwa moja masuala ya mazingira na umaskini. Sasa hivi bajeti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira imeongezeka kutoka shilingi 1,076,707,300 mwaka 2005/06 hadi kufikia shilingi 5,675,971,000 mwaka 2006/07. Mfumo-mkakati wa kugawa bajeti sasa hivi unahusisha uhakiki wa mipango ya matumizi ya sekta ya umma na MKUKUTA kwa namna ambayo vyote huzingatia matokeo na kufafanua majukumu ya wizara mbalimbali, idara na wakala wa serikali. Yote haya yamesaidia kutoa MKUKUTA kutoka katika maono ya wanamipango kuelekea katika matumizi halisi.

## Maandalizi ya Sheria ya Mazingira na Mchakato wa MKUKUTA

Wakati watanzania wanaendelea na mchakato wa kutayarisha MKUKUTA, maboresho ya muundo wa taasisi za kusimamia mazingira na kuandaa sheria ya mazingira yalikuwa yanafanyika. Mahusiano baina ya mazoezi haya mawili yalikuwa muhimu ili kushawishi utendaji wa mamlaka za mazingira, ujumuishaji wa mazingira katika MKUKUTA na kutimiza madhumuni ya kupunguza umaskini.

Wadau waliohusika katika mandalizi ya sheria ya mazingira, pia walishiriki katika warsha za MKUKUTA. Mbinu hii ilisaidia kupunguza migongano na kuweka bayana mchango wa mazingira katika harakati za kuondoa umaskini. Matokeo yake ni kuwa baadhi ya mambo yanayopaswa kufanyika kupitia MKUKUTA, yanaunga mkono utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ikiwa ni pamoja na ukuzaji wa uwezo wa kusimamia mazingira katika serikali za mitaa na kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa viashiria vya umaskini na mazingira.

Sheria ya mazingira imeweka misingi ya kisheria ya utunzaji, usimamizi wa mazingira na ufafanuzi wa madaraka na majukumu ya mamlaka zinazosimamia mazingira. Pia umeweka msingi wa uhusishaji wa mipango ya mazingira na upunguzaji wa umaskini kwa:

- Kuweka mkazo katika kuboresha mazingira na maisha ya watu maskini.
- Kufanya suala la tathmini ya kimkakati na ile ya athari za shughuli za maendeleo katika mazingira kuwa la kisheria.

- Kukusanya taarifa za hali ya mazingira nchini kuwa la kisheria.
- Kuzitaka idara, wizara na taasisi za serikali kuanzisha vitengo vyao vya usimamizi wa mazingira.

## Maandalizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Umaskini

Ili kupunguza umaskini, viashiria vya kupima umaskini ni lazima vibainishwe. Mwaka 2001 Serikali ilianzisha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa umaskini wenye madhumuni ya kuweka utaratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Hata hivyo viashiria vya mazingira havikuwemo licha ya kuwa mazingira ni tegemeo la watu. Hali hii ilipelekea kufanyika kwa utafiti kwa ajili ya kuandaa viashiria sahihi vya umaskini na mazingira na kuboresha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa umaskini ili kuhakiki utekelezaji wa MKUKUTA katika ngazi zote.

**Sanduku Na. 3.**
**Viashiria vya Mazingira vya kufuatilia utekelezaji wa MKUKUTA**

| | |
|---|---|
| **Lengo** | Kuchochea maendeleo endelevu yaliyo kamilifu |
| **Kiashiria** | Idadi ya kampuni zinazofanya tathmini ya athari ya Mazingira na zinazofuata kanuni za Mazingira |
| **Lengo** | Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake vijijini na mijini |
| **Kiashiria** | Asilimia ya kaya ambazo kipato kikuu kinatokana na uvunaji, usindikaji na uuzaji wa mazao ya maliasili |
| **Lengo** | Utoaji wa nishati ya uhakika na yenye bei nafuu kwa wateja |
| **Kiashiria** | Asilimia ya kaya za vijijini na mijini zinazotumia vyanzo mbadala vya nishati tofauti na kuni (ikiwa ni pamoja na mkaa) kama chanzo kikuu cha nishati<br>Ongezeko la upatikanaji wa maji safi, yanayotosha na salala; usafi, makazi bora na mazingira salama na endeolevu. |
| **Viashiria** | Idadi ya watu wanaotumia maji ya bomba au vyanzo vya maji vilivyohifadhiwa kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa<br>Asilimia ya kaya zenye miundombinu ya usafi<br>Asilimia ya shule zenye miundombinu ya usafi kwa (mujibu wa sera)<br>Idadi ya milipuko ya kipindupindu iliyoripotiwa<br>Ukubwa wa eneo la maliasili linalosimamiwa na wananchi/ mashirika ya kijamii |
| **Lengo** | Muundo na mifumo ya utawala pamoja na sheria kwa pamoja ni za kidemokrasia shirikishi, zenye uwakilishi na uwajibikaji |
| **Viashiria** | Asilimia ya wanawake kutoka katika kaya za wakulima wadogo wanao miliki ardhi kimila au hatimiliki<br>Jumla ya mapato yatokanayo na kodi, ada na leseni za maliasili (misitu, uvuvi, wanyamapori na uchimbaji wa madini) |

# Mabadiliko katika mfumo wa misaada – Tanzania kuongoza maamuzi ya misaada ya maendeleo

Nchi nyingi zinazoendelea zimekuwa zikipokea maelekezo ya wafadhili katika kupanga mipango ya maendeleo. Ingawa ni wazi kwamba maskini wanategemea rasilimali zilizo katika mazingira kwa maisha yao lakini wafadhili wachache walitoa kipaumbele katika masuala ya mazingira. Waliofanya hivyo walikuwa na madhumuni ya kutangaza rasilimali ambazo ni urithi wa dunia hata kama hazisaidii wakazi wa maeneo hayo. Hali hii haikusaidia kuendeleza matakwa ya nchi husika katika hifadhi ya mazingira ili kuleta maendeleo endelevu.

## Ushawishi wa Tanzania kwa wafadhili

Katika miaka ya 1980 na 1990 mahusiano baina ya Tanzania na wafadhili yalitawaliwa na hali ya utegemezi na migongano kati ya nchi yetu na wafadhili katika maeneo ya sera na utawala. Sasa hivi hali imebadilika na kufanya nchi kutoa kipaumbele na kuwa na maamuzi katika mipango ya maendeleo. Hii ni pamoja na kuandaa muundo wa kitaifa wa upokeaji wa misaada kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kuanziasha mkakati wa mfuko wa pamoja wa wafadhili. Wakati wa kuandaa MKUKUTA Tanzania ilitumia mtindo huu ili kudhibiti mchakato kwa mara ya kwanza.

## Uratibu mzuri wa Wafadhili na Wanaharakati wao wa Mazingira

Wafadhili walibadilisha mtindo wa misaada, kwa kufuata matakwa ya nchi na malengo ya Maendeleo ya Milenia. Kitengo cha ufadhili cha taasisi ya Maendeleo ya Uchumi (OECD) kilitoa maelekezo ya muundo wa kuhakikisha kuwa misaada inafaa bila kuingilia matakwa ya nchi. Hali hii ilipata msukumo kutoka kwa Rais wa awamu ya tatu – Benjamini Wiliam Mkapa ambaye alifuatilia kwa karibu suala hili ikiwa ni pamoja na utetezi aliyoufanya kule Roma - Italia na Paris – Ufaransa kuhusu umuhimu wa nchi husika kuwa mstari wa mbele katika kujiletea maendeleo. Wafadhili hawakutoa maamuzi wakati wa MKUKUTA bali walisaidia kwa kutoa hoja katika mambo yafuatayo:

- Baada ya kuridhika na maamuzi ya vikundi vya wafadhili wenye ushawishi mkubwa wa nchi tajiri wanaoitwa kikundi cha Roma na Paris, waliiachia Tanzania kusimamia mchakato wa MKUKUTA pasipo kuingiliwa.
- Ingawa wafadhili wana mitazamo na malengo yao, misaada mingi sasa imehuishwa na kufuata maelekezo na bajeti ya serikali.
- Pamoja na kutohusika moja kwa moja kubaini masuala ya msingi katika MKUKUTA, wafadhili walitoa maoni yao kupitia Umoja wa Wafadhili na wameendelea kushiriki katika utekelezaji wa programu mbalimbali za masuala ya umaskini na mazingira.

Kwa ujumla mchakato wa ujumuishaji wa mazingira katika MKUKUTA haukutawaliwa na wafadhili, hivyo tunaweza kusema hali ya kujitegemea imeanza kufufuka katika Tanzania, na ni mfano mzuri wa namna wafadhili walivyoweza kujipanga na kuunga mkono nia ya Tanzania ya kujitegemea.

# Mbinu zinazofaa katika harakati za kujumuisha masuala ya mazingira

Mkakati wowote wa kitaifa lazima ukubalike na wadau na ili kufanikisha jambo hili, inabidi kuwepo: uhusiano mzuri kati ya wadau, zipatikane taarifa na uchambuzi wa kina kwa masuala yote muhimu, mawasiliano kuhusu mchakato unaotumika na utaratibu wa maamuzi uwekaji vipaumbele yawe bayana. Katika Sura hii tunaeleza kwa ufupi mbinu zilizotumika katika mchakato wa MKUKUTA kufanikisha mambo hayo. Baadhi ya mbinu hizo zilikuwa maalum kwa ujumuishaji wa masuala ya mazingira (hasa taarifa, uchambuzi na mawasiliano). Mbinu hizi zilizotumika katika mchakato wa MKUKUTA zimesaidia watu wengi kufahamu vizuri masuala ya mazingira.

## Mbinu za mashauriano katika kufanikisha ushirikishwaji wa wadau


*Ni jambo la muhimu kwa mikakati kuandaliwa na wale ambao watasimamia mabadiliko yanayokusudiwa* – Hii ndio changamoto ya mwanzo wakati wa kuandaa mkakati wa kitaifa kama vile MKUKUTA. Mchakato wa MKUKUTA uliweza kuikabili changamoto hiyo kwa kushirikisha wadau wa aina mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa na Asasi za Kijamii. Hii inatofautisha mchakato wa MKUKUTA na Mkakati wa Mwanzo wa kupunguza Umaskini (Poverty Reduction Stratergy 2000). Baadhi ya wadau walioshirikishwa ni pamoja na:

- Serikali za mitaa – kwa kuendesha mikutano ambayo ilihusisha watu takriban 18,000 katika vijiji 168 (wastani wa vijiji vinne katika kila wilaya);
- Mashirika ya kijamii – kwa kuwezesha majadiliano ambayo watu 1,000 walishiriki;
- Umma-madodoso 25,000 yalijazwa na kurejeshwa;
- AZISE za kimazingira- kwa kutoa makala; na
- Wabunge – kwa majadiliano ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira na ushauri wa Wabunge wakati wa mijadala Bungeni.

***Mchakato wa mashauriano ulitumia muda na gharama kubwa***
Katika michakato ya sera zilizotangulia, serikali ndiyo ilikuwa msimamizi mkuu wa mashauriano. Hali hii imebadilika kwa kushirikisha wadau wote. Kwa kuwa dhana hiyo ni mpya, mafanikio ya mashauriano hayakupatikana kwa urahisi. Hivyo, serikali iliamua kwa kupitia sekretariati ya MKUKUTA, iliendesha warsha ya kuelimisha umma juu ya umuhimu wa wadau na sekta mbalimbali kutoa maoni yao, na kisha kuandaa mwongozo wa mashauriano.

*Pia mashauriano maalumu ya uhusiano wa umaskini na mazingira yalifanyika* – Programu ya Ujumuishaji wa Masuala ya Mazingira katika Mkakati wa kuondoa

**Mchoro Na. 1.** Awamu tatu za Mashauriano katika maandalizi ya MKUKUTA



*Mashirika ya dini yalishirikishwa kwa ukamilifu* – Mashirika ya dini yalishiriki katika kutoa maoni yao.

*Madodoso pia yalitumika kupata maoni ya watu binafsi* – Madodoso 500,000 yaliyosambazwa kwa watu mbalimbali, 25,000 yalijazwa na kurejeshwa, na kufanyiwa uchambuzi wa kina na kitengo cha Taifa cha Takwimu.

*Mashauriano yalisanifiwa ili kukusanya, kuimarisha na kulenga kwenye masuala muhimu yanayochangia kuleta maendeleo* – Awamu tatu za mashauriano zilifanyika kwenye ngazi ya wilaya (kielelezo Na.1).

***Changamoto zilizojitokeza wakati wa Mashauriano***

*Awamu zote za mashauriano na utafiti zilikuwa mzigo mkubwa kwa serikali kiasi ambacho kilivuka maandalizi ya serikali* – Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha mafunzo ya wawezeshaji wa Serikali za Mitaa (yaliyohusisha maafisa maendeleo ya jamii wawili kutoka kila mkoa). Hata hivyo, utekelezaji haukuwa kamilifu kama ilivyotarajiwa.

*Mrejesho wa mashauriano ya watu binafsi ulikuwa mdogo* – Hapakuwa na mrejesho wa matokeo ya mashauriano kwenye vijiji, ijapokuwa kulikuwa na mrejesho kiasi kwa maagizo maalum kupitia kwenye vyombo vya habari hususan redio na wakati wa Wiki ya Umaskini.

*Matokeo ya mashauriano hayo yalielekea kuthibitisha matokeo ya tathmini shirikishi ya umaskini iliyofanyika awali* – Ukosefu wa huduma za msingi ikiwa ni pamoja na maji na nishati, utekelezaji duni wa sheria (hasa sheria za ajira, ardhi na mazingira), na ukosefu wa mitaji ndiyo matatizo makubwa yaliyojitokeza. Karibu masuala yote yaliyojitokeza katika mashuriano yalizingatiwa katika mchakato wa MKUKUTA.

*Mchakato wote wa mashuriano uliwasaidia wadau kufikiria upya vipaumbele vyao* – Matokeo ya awamu zote tatu za mashauriano yalilenga kuwawezesha wadau kujifunza, na ikibidi, kubadili mtazamo. Mfano halisi ni AZISE za kimazingira, ambazo baadhi ya vipaumbele vyao viliegemea zaidi katika uhifadhi na ulinzi wa mazingira bila kuzingatia matumizi bora ili kuinua hali ya maisha yao. Kwa ujumla, mashauriano yamewawezesha wadau kujifunza na kuwa na ushirikiano miongoni mwao. Tunaamini kwamba mchakato huu umetimiza dhana kuu ya Watanzania ya '*umoja*'.

## Taarifa na uchambuzi – Changamoto za mahusiano ya umaskini na mazingira

*Mchakato wa MKUKUTA pia ulihusu unyambulishaji, uchambuzi, usambazaji na usimamizi wa taarifa* – Taarifa muhimu zilitokana na majadiliano, sio nyaraka. Hii ilitokana na uwezo wa wadau na vipaumbele walivyojiwekea. Maoni ya AZISE zinazojihusisha na masuala ya mazingira, yalijumuishwa.

*Ofisi ya Makamu wa Rais ilitafuta wataalam washauri wa muda kufanya tafiti za uhusiano wa umaskini na mazingira* – Watafiti hao walitumia takwimu sahihi zinazoonyesha mwelekeo unaobainisha mahusiano kati ya mambo hayo. Baadhi ya matokeo yamedhihirisha kuwa ni ya muhimu sana, hususan uchambuzi wa takwimu uliolenga kwenye Tahakiki ya Matumizi ya Umma (Public Expenditure Review) na Taarifa ya Benki ya Dunia ya Uchumi wa Tanzania. Uchambuzi wa takwimu hizo ulionyesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ustawi wa jamii na mazingira, pamoja na kiasi cha mapato ya maliasili ambayo serikali ilikuwa inapoteza (sura ya Pili). Tafiti nyingine zililenga kwenye mbadala zinazoweza kutumika baadaye, kwa mfano, utafiti wa umuhimu wa tathmini madhubuti ya masuala ya mazingira kwa ajili ya kuboresha upangaji wa maendeleo, na utafiti wa viashiria vya uhusiano wa umasikini na mazingira.

*Wachambuzi walikuwa Ofisi ya Makamu wa Rais na Timu ya Uandishi wa MKUKUTA* – Kwa kutumia mchakato wa wadau mbalimbali ambao waliwezesha kupatikana kwa taarifa, changamoto kuu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa kusanisi maoni. Aidha, wataalam walichambua pia taarifa katika maandiko (ambayo kwa kiasi kikubwa ni ya kimataifa) inayohusu uhusiano wa umaskini na mazingira. Taarifa hizo zilichambuliwa kulingana na mazingira ya Tanzania.

*Katika mchakato wote kazi kubwa ilikuwa ni kuanzisha utaratibu wa utunzaji wa taarifa* – Katika mchakato wa MKUKUTA taarifa nyingi zilipatikana. Tatizo lililojitokeza ni utunzaji wa taarifa hizo, ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi. Changamoto hii itarejewa tena katika sura ya Saba.



## Kuyapa mazingira kipaumbele

Suala la mazingira limekuwa halipewi umuhimu unaostahili katika mipango ya maendeleo. Mawasiliano ya karibu yalihitajika ili kushirikisha wadau na kuwa na uelewa wa pamoja wakati wa mchakato. Hivyo basi, wadau wengi walioshirikishwa katika kazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya kujumuisha masuala ya mazingira wakati mwingine walielezea kazi yao kama shughuli ya mawasiliano, iliyolenga kuboresha uelewa, kuleta mvuto na utashi wa kisiasa katika kushughulikia masuala ya umaskini na mazingira: Mbinu zilizotumika ni pamoja na:

- *Mbinu, Midahalo na lugha.* Lugha iliyotumika ilihusisha masuala ya mazingira yanavyohusiana na changamoto nyingine za maendeleo kama afya, elimu, kipato, ustawi na usalama.
- *Miongozo.* Kuandaa vigezo, miongozo na viashiria vya kubainisha uhusiano wa mazingira na umaskini ili kuwasaidia wadau kutoa maoni yao na kufanya uchambuzi.
- *Uwazi:* Kurahisisha upatikanaji wa nyaraka za MKUKUTA kwa wadau ili kuendeleza mchakato.
- *Mashirika ya dini.* Kupanua wigo wa mtandao wa MKUKUTA ili kufikia wadau wengi zaidi.

- *Vyombo vya habari.* Vyombo vya habari vilishirikishwa ili kuhakikisha vinafikisha ujumbe kwa walengwa.
- *Uhamasishaji wa umma:* Kutoa habari kupitia majarida, vipeperushi. na njia nyingine za mawasiliano.

*Kuutambulisha MKUKUTA* – Kukua kwa uelewa wa mchakato wa MKUKUTA kulileta ongezeko la matarajio ya umma juu ya kupunguza umaskini. Ujio wa neno MKUKUTA uliongeza hamasa na ari na watu kutaka kujua undani wake na hivyo kufanya likubalike. Hii ilikuwa tofauti na PRS, ambayo ilihusishwa na matakwa ya wafadhili.




**Kuingiza Hoja za Mazingira Katika Duru za Kisiasa Tanzania Imekuwa Jambo Nzuri**

## Maamuzi ya kubainisha vipaumbele

Maamuzi wakati wa mchakato wa MKUKUTA yalifuata utaratibu unaofuatwa katika maandalizi ya mipango mingine ya kitaifa kama ifuatavyo:

- *Baraza la mawaziri:* Hiki ni chombo kilichotoa idhini ya mwisho.Waraka wa Baraza la Mawaziri uliandaliwa na kuwasilishwa. Baada ya kuupitia Baraza lilitoa maelekezo ya marekebisho na yalipokamilishwa uliidhinishwa.
- *Kamati ya ufundi ya Makatibu Wakuu* – ilitoa ushauri kuhusu ubora wa uchambuzi na mapendekezo kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri - pamoja na kujumuisha shughuli za MKUKUTA katika mchakato wa bajeti.
- *Kamati ya tahariri* – iliamua juu ya muundo wa jumla wa waraka na uwekaji wa vipaumbele. Ushirikishaji wa makatibu wakuu watatu wenye ushawishi mkubwa katika timu ya tahariri uliharakisha mchakato.
- *Kamati ya uandishi ya MKUKUTA* – ilitoa rasimu ya MKUKUTA baada ya kujadiliana na wadau namna ya kuuwasilisha.

Kwa kawaida uwekaji wa vipaumbele katika mipango hasa inapohusisha wadau wengi huwa sio rahisi. Katika MKUKUTA uwekaji wa vipaumbele ulifuata misingi mitatu:

- *Kanuni za utayarishaji mipango ya Kimkakati* – Baadhi ya kanuni hizo ziliwezesha ubainishaji wa vigezo vya uwekaji wa vipaumbele hususan vinavyohusiana na haki za binadamu, masuala ya kiuchumi na urekebishaji wa miundo, ushirikiano baina ya sekta, ugatuzi wa madaraka, na uanishaji wa masuala mtambuka.
- *Mashauriano ya kina yanayohusisha wadau wengi* – yatakuwa ndiyo njia kuu ya uwekaji wa malengo na vipaumbele vya wadau vinavyoonyesha mahitaji, kiasi cha msaada unaohitajika na vigezo vinavyopima mafanikio.
- *Kulenga kutatua changamoto za nchi* – Katika mchakato wote wa MKUKUTA maamuzi yalifanywa kwa kuzingatia matatizo ya Tanzania na kushirikisha wadau wazawa wengi iwezekenavyo na njia zinazowezesha kuwafikia kwa urahisi. Aidha, juhudi zilifanyika kuhakikisha kila mdau anapata mrejesho. Serikali iliweka msimamo bayana wa kuboresha ustawi na utawala na kuahidi kusimamia kwa kikamilifu ufanikishaji wa malengo na vipaumbele vilivyoainishwa.

Ijapokuwa misingi hii matatu iliweka mwongozo wa jumla, masuala yaliyojitokeza kadri mchakato ulivyoendelea yalijadiliwa kulingana na uzito wake.



*Majadiliano ya wadau wa sekta mbalimbali* yalikuwa ya manufaa kwa sababu kila suala lilijadiliwa kwa kina kwa kutumia vigezo muhimu vya uchambuzi. MKUKUTA haukuwa hasa mchakato wa kiufundi isipokuwa wa kisiasa zaidi, ambapo maoni ya wadau ya hali halisi ndiyo yaliyotoa vipaumbele kulingana na vigezo vilivyowekwa.

*Kadri kazi ilivyokuwa ikikamilika, mgawanyo wa kisekta kwa kutumia jedwali uliwezesha kuainisha mafungu ya masuala yanayofanana.* Mafungu haya yalihusishwa na Mradi wa Milenia wa mwaka 2002 ambao ni mradi wa kimataifa wa kuhakiki utekelezaji wa kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

*Hatimaye, mchakato wa MKUKUTA uliainisha malengo* 108. Malengo haya yaliachwa hivyo mpaka wakati wa utekelezaji. Aidha, masuala ya mazingira pamoja na masuala mengine mtambuka yaliwekwa bayana katika malengo haya. Suala la malengo linajadiliwa tena katika sura ya Saba, wakati wa kuangalia changamoto ya kubainisha njia inayofaa kutumika kutimiza malengo hayo 108 ya MKUKUTA.

# Tathmini ya matokeo ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira mpaka sasa

Ingawa ni mapema kutoa maoni ya uhakika kuhusu matokeo ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika MKUKUTA, tayari kuna ishara tosha inayodhihirisha utashi wa kuyapa mazingira kipaumbele. Malengo ya mazingira yaliyowekwa katika MKUKUTA na mijadala ya mazingira inayoendelea inadhihirisha mabadiliko ya kifikra na kisera kuhusu mchango wa mazingira katika maendeleo endelevu na utawala bora. Hali hii inatokana na masuala yafuatayo.

## Malengo ya mazingira yaliyomo katika MKUKUTA

Masuala ya mazingira yameainishwa katika malengo ya MKUKUTA katika makundi yafuatayo:

- *Malengo ya mazingira*. Malengo 15 kati ya 108 katika MKUKUTA yanahusu utendaji wa moja kwa moja (jedwali Na. 2); na malengo matano yanahusu utendaji unaohusiana na masuala ya mazingira.
- *Shughuli za mazingira*. Kuna shughuli zisizo za mazingira lakini zinachangia katika udhibiti na hifadhi ya mazingira, kwa mfano shughuli za upatikanaji na udhibiti wa maliasili na utawala bora (utoaji na upokeaji rushwa), hasa uvunaji haramu wa magogo.
- *Ufuatiliaji wa masuala ya mazingira*. Viashiria vya kufuatilia mwenendo wa umaskini na mazingira vimeandaliwa kwa ajili ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA.



Ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mchakato wa MKUKUTA umesaidia kuainisha umuhimu wa mazingira na masuala mengine mtambuka. Aidha malengo yote yamezingatia utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi (2005) na sera ya mazingira. Pia, Kamati ya Mawaziri wanaohusika na usimamizi wa mazingira imeanzishwa.

## Matokeo ya Pili – Mabadiliko chanya katika mijadala inayohusu mazingira na umaskini

Ni muhimu kufahamu masuala ya mazingira yaliyopewa kipaumbele na yale ambayo yalionekana kuwa changamoto katika mchakato wa MKUKUTA. Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 iliainisha na kufanya uchambuzi ambao ulionyesha kwamba umaskini na idadi ya watu ndio sababu kuu za uharibifu wa mazingira.

Kwa kawaida umaskini unasababisha uharibifu wa mazingira kwa kupunguza uwezo wa watu kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali. Kwa lugha nyingine uhifadhi haukuchuliwa kama mbinu ya kufanikisha malengo ya kuboresha maisha kwani unaonekana kudhibiti matumizi ya maliasili. Imani hii imebadilishwa katika MKUKUTA (Sura ya Pili); kwa kuonyesha uwiano kati ya matumizi endelevu ya maliasili na ustawi wa jamii pamoja na ukuaji wa uchumi. Hivi sasa kuna masuala ya mazingira yaliyothibitishwa kuboresha ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi na hivyo kuwa mambo la msingi kisheria na kiuchumi.

Hata hivyo, utashi wa kisiasa, mgawanyo wa mapato kwa usawa na uwekaji wa mbinu za kudhibiti madhara ya kijamii na utawala bora ni mambo muhimu katika kufanikisha malengo yaliyo katika MKUKUTA (Waldman 2005).

Pamoja na kuweka msisitizo zaidi kwenye mazingira na masuala mengine mtambuka kuliko katika mikakati ya kuondoa umaskini iliyotangulia, MKUKUTA unazingatia vielelezo vingi vya maendeleo. Msisitizo wa ustawi wa kiuchumi na mbinu zinazoongozwa na soko bado una manufaa katika kufanikisha malengo ya MKUKUTA. Ijapokuwa MKUKUTA haujazungumzia uwezo wa kiikolojia, lakini umejumuisha masuala ya msingi kama vile haki za binadamu na ustawi wa jamii ili kuendeleza mjadala unaoonyesha umuhimu wa mazingira katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Jedwali Na. 2.** Malengo ya mazingira katika MKUKUTA

| | |
|---|---|
| **Nguzo ya kwanza: Kukua kwa Uchumi na kupungua kwa umaskini wa kipato** | |
| **Lengo** | **Malengo ya mazingira** |
| 2. Kuboresha ukuaji wa uchumi kwa ujumla | 1. Kupunguza athari za mazingira katika maisha ya watu<br>2. Kupunguza uharibifu wa ardhi na upoteaji wa bioanuai |
| 4. Kupunguza umaskini wa kipato kwa watu wote (wanaume na wanawake) vijijini | 3. Ongezeko la kipato cha jamii vijijini kutokana na shughuli za matumizi ya maliasili (k.m wanyamapori, misitu samaki n.k.) |
| **Nguzo ya pili: Kuboreka kwa hali ya maisha na ustawi wa jamii** | |
| **Lengo** | **Malengo ya mazingira** |
| 3. Upatikanaji wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama, kuongezeka kwa idadi ya watu wenye nyumba bora; na kupungua kwa madhara ya mazingira | 4. Idadi ya watu wanaopata maji safi na salama katika maeneo ya vijijini, ikiwa ni pamoja na kutumia muda kidogo zaidi kuchota maji hayo, kutoka asilimia 53 katika kipindi cha mwaka 2003 mpaka asilimia 80 katika kipindi cha mwaka 2009/10<br>5. Ongezeko la uwiano wa watu wanaopata maji safi na salama katika maeneo ya mijijini, ikiwa ni pamoja na kutumia muda kidogo zaidi kuchota maji hayo, kutoka asilimia 73 mwaka 2003 mpaka asilimia 90 mwaka 2009/10<br>6. Ongezeko la upatikanaji wa huduma bora za majitaka katika maeneo ya mijini kutoka asilimia 17 mwaka 2003 mpaka asilimia 30 katika mwaka 2010<br>7. Kupungua kwa idadi ya kaya zinazoishi katika maeneo yasiyo rasmi<br>8. Shule zote kuwa na miundombinu ya usafi ifikapo mwaka 2010<br>9. Asilimia 95 ya watu kuwa na miundombinu muhimu ya usafi ifikapo mwaka 2010<br>10. Kupungua milipuko ya kipindupindu kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2010<br>11.Kupunguza uchafuzi wa maji kutoka asilimia 20 mwaka 2003 mpaka asilimia 10 ifikapo mwaka 2010<br>12. Kupunguza Uchafuzi unaotokana na shughuli za viwanda na kilimo<br>13. Kupunguza uwezekano wa kutokea majanga ya kimazingira<br>14. Kuboreka kwa rasilimali za ardhi, misitu na mifumoikolojia ambayo jamii inategemea kwa maisha<br>15. Kupungua kwa uharibifu wa ardhi na upoteaji wa bioanuwai |

## Matokeo ya Tatu – Njia shirikishi ya kuanzisha mchakato wa kujumuisha masuala ya mazingira katika shughuli na mipango ya maendeleo ya baadaye

Mchakato wa kuandaa MKUKUTA ulikuwa na manufaa na ulitoa fursa kwa wadau kujadili kwa kina masuala yanayohusu uhusiano uliopo kati ya umaskini, mazingira na maendeleo endelevu kama ifuatavyo:

- Kuandaa mbinu zinazolenga katika matokeo ya jumla badala ya matokeo ya kisekta.
- Kujumuisha masuala mtambuka na hivyo kuweka uhusiano thabiti katika utekelezaji na utendaji katika masuala ya kisekta pamoja na ushawishi na ushiriki wa vikundi vya kimazingira.
- Kukuza ari ya kujitegemea na uwajibikaji katika ngazi zote.
- Kuwasilisha makubaliano ya kitaifa badala ya utaratibu wa mpango wa serikali – katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa na upunguzaji wa umaskini.
- Kufanikisha mshikamano wa kweli kati ya wadau mbalimbali kuhusu masuala muhimu ikiwa ni pamoja na mazingira.
- Kusimamia mchakato wa mabadiliko kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wafadhili.
- Kuunganisha utekelezaji na ufuatiliaji wa MKUKUTA na bajeti.
- Kuhusisha taasisi muhimu katika masuala ya mazingira na umaskini – hasa Wizara ya Fedha na taasisi nyingine kupitia Kikundi cha Mashauriano kuhusu Mazingira (Environmental Working Group).
- Kuendeleza mbinu shirikishi inayosikiliza maoni ya watu wote.

*Mafanikio ya mchakato wa MKUKUTA yametokana na ushirikishwaji wa wadau wengi hususan wanaharakati wa mazingira.* Hapo awali uandaaji wa mikakati na mipango ya serikali ulikuwa na urasimu uliofanya mafaniko ya mipango hiyo kutokuwa ya kuridhisha licha ya kutoa mwanya kwa mashirika ya kijamii na wafanyabiashara kushinikiza kwa maslahi yao. Mchakato wa MKUKUTA umeonyesha:

- Dhamira ya kweli ya serikali kuleta mabadiliko na kushughulikia matatizo ya umaskini na mazingira.




**Harakati za kujumuisha mazingira katika harakati za maendeleo zinahitaji muda wa kutosha**

- Mchakato wa MKUKUTA ulipata msukumo kutokana na uchaguzi wa mwaka 2005.
- Sekta zilitambua kwamba mgawanyo wa bajeti utafuata malengo ya MKUKUTA.

## Matokeo ya Nne – Mabadiliko ya Kitaasisi na utawala

Mchakato wa MKUKUTA umeonyesha mafanikio kwa jinsi wadau walivyobadilika na kuanza kujumuisha masuala ya mazingira katika mipango na bajeti zao. Kwa mtazamo huu, uzoefu wa Tanzania kuhusiana na mabadiliko ya sera na taasisi katika ujumuishaji wa masuala mtambuka umekuwa tofauti na unaotumika katika nchi nyingi zinazoendelea.

Serikali imeanza kubadilika kwa kuanza na hatua ya Ofisi ya Makamu wa Rais/ Idara ya Mazingira kwa kutoa "*Mwongozo wa Uhuishaji wa Masuala ya Mazingira katika Mipango na Bajeti za Sekta na Serikali za Mitaa*". Mwongozo huu unajumuisha mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na jinsi ya kusaidia jamii, kupanua wigo wa kuendeleza mijadala, kutatua matatizo kwa kutumia njia asilia, kuandaa taarifa, na kutumia viashiria vya uhusiano kati ya umaskini na mazingira.



**Baada ya kukua kwa uelewa, elimu ya mazingira imejumuishwa katika mitaala ya elimu**



Masuala ya mazingira yanajumuishwa katika mitaala ya elimu kwa kutumia Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Mazingira na Mawasiliano.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Management Council ) limeongeza jitihada yake ya uhamasishaji kwa kushirikiana na sekta nyingine. Pia kuna ongezeko la shughuli za AZISE za mazingira, ikiwa ni pamoja na kusaidia katika shughuli za kuongeza kipato na uzalishaji kwa mfano, upandaji wa miti na ukusanyaji wa taka ngumu, shughuli ambazo hivi sasa zinatengewa mafungu katika bajeti ya serikali. Aidha, kutokana na ongezeko la uchafuzi wa mazingira serikali iliweka kodi kwenye uagizaji wa mifuko ya plastiki na kupiga marufuku baadhi ya bidhaa za plastiki kuingizwa nchini.

Huu ni mwanzo mzuri wa kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za maendeleo.

# Changamoto za Utekelezaji

Kwa kiasi kikubwa MKUKUTA umetatua tatizo la upangaji wa mipango isiyo shirikishi na kufanya MKUKUTA uwe mpango uliokubalika na wadau wote. Kutokana na maelezo ya awali inabashiriwa kuwepo changamoto zinazohusiana na utekelezaji wake, ikiwa ni pamoja na uwekaji wa vipaumbele vya kisekta, ambavyo vitatilia mkazo masuala ya utawala bora, sera na sheria ya mazingira na jinsi ya kuhamasisha uwekezaji.

## Vipaumbele katika malengo ya MKUKUTA

Hii ni changamoto inayotokana na ukweli kwamba, MKUKUTA una malengo zaidi ya mia moja (100), ambayo yote ni muhimu kulingana na matakwa ya kuboresha maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Hivyo, uchaguzi wa vipaumbele vya kuanzia itategemea wadau husika. Rais Kikwete akihojiwa na gazeti la "The Economist" mwezi Septemba mwaka 2006, alitumia zaidi ya saa moja kufafanua mahitaji ya Tanzania kama yalivyoainishwa katika MKUKUTA. Hii inaonyesha jinsi ambavyo masuala ya mazingira kupewa kipaumbele itaendelea kuwa changamoto.




**Changamoto kubwa ni kubainisha uwiano sahihi ili kukidhi mahitaji muhimu yanayohitaji matumizi ya ardhi**

Kwanza, ni muhimu kuhakikisha kwamba mifumo ya uwekaji wa vipaumbele inazingatia masuala ya uhusiano wa umaskini na mazingira na haitoi misamaha ya kodi isiyo ya lazima kwa uwekezaji wa muda mrefu. Pili inabidi watekelezaji waoneshe uhusiano uliopo kati ya ubora wa mazingira na maisha ya kila siku ya jamii. Tatu, mipango ioneshe jinsi utekelezaji utakavyokabiliana na madhara ya kimazingira kwa mfano mabadiliko ya tabianchi na mengineyo. Aidha, matumizi ya rasilimali katika kutekeleza malengo ya kisekta lazima yazingatie umuhimu wa rasilimali hiyo kwa sekta nyingine. Kwa mfano, katika MKUKUTA, lengo mojawapo ni kukuza kilimo cha umwagiliaji (kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuboresha usalama wa chakula). Ili lengo hili lifanikishwe upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji ni jambo la lazima. Pia maji yanahitajika katika sekta ya nishati kwa kuzalisha umeme. Huu ni mfano mmojawapo unaoonyesha changamoto katika utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA na kudhihirisha umuhimu wa wadau kushirikiana katika uwekaji wa vipaumbele katika utekelezaji.

## Uzingatiaji wa Sera za kisekta katika MKUKUTA na Sheria ya Mazingira

*MKUKUTA na Sheria ya Mazingira vinawiana*

Hivi sasa Tanzania inakabiliwa na changamoto ya utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA ambayo yanasisitiza matumizi ya mazingira ili kujinusuru na umaskini kwa kutumia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ambayo inasisitiza matumizi endelevu ya rasilimali. Utekelezaji wa masuala haya mawili ni mojawapo ya changamoto ambazo zimekwisha bainishwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Changamoto nyingine ni uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvamizi wa wafugaji katika vyanzo vya maji; kilimo katika maeneo ya miinuko mikali ya milima; ukataji holela wa miti kwa ajili ya biashara ya magogo; na migogoro mingine inayohusiana na matumizi ya ardhi. Kimsingi, eneo husika linapaswa kufanya maamuzi kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali ili kujiletea maendeleo huku likizingatia utekelezaji wa sheria ya mazingira.



**Mizinga ya Asali katika Mbuyu: Maliasili ni muhimu sana katika maisha ya kawaida vijijini**



Katika utekelezaji wa MKUKUTA na Sheria ya Mazingira, kuna masuala muhimu yanayohitaji mjadala na maamuzi ya kitaifa kuhusu shuguli zipi za kiuchumi ziendelee ili kunusuru mazingira na kuepusha madhara yanayoweza kulipata taifa baadaye. Itatubidi kuhakikisha kwamba mazingira yanakuwa ndiyo kiini cha kipimo cha maendeleo. Maoni na michakato iliyotolewa na MKUKUTA pamoja na kazi ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira yametoa ulingo wa majadiliano ya mustakabali wa mazingira ya taifa letu.

## Utawala bora katika utekelezaji wa MKUKUTA na Sheria ya Mazingira

Benki ya Dunia ilishauri kuwa utawala bora katika matumizi ya maliasili ni jambo muhimu katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu nchini Tanzania. Ushauri huu unawiana na lengo la MKUKUTA ambalo linategemea sana utawala bora katika usimamizi wa mazingira, hasa kwa wadau ambao kimaisha wanategemea mazingira. Hii inamaanisha kwamba ipo haja ya kuweka nguvu zaidi katika jitihada ya ushirikishwaji wa shughuli za usimamizi wa maeneo ya misitu na wanyampori na rasilimali nyingine kuliko ilivyo hivi sasa. Maeneo mengi ya

mifumoikolojia hiyo, yanaweza kuendelezwa vizuri zaidi kwa kutumia mashirika ya kijamii ili kujumuisha uzoefu wao katika masuala ya umaskini na mazingira yaliyomo katika nguzo tatu za kisekta za MKUKUTA. Kwa kiasi kikubwa maendeleo ya MKUKUTA na Sheria ya Mazingira yamekuwa yanaamuliwa na wataalam waliobobea na serikali kuu. Hivi sasa, busara zaidi, dhamira na mabadiliko ya tabia yanahitajika katika ngazi zote. Hivyo, asasi za kiraia na serikali za mitaa zinapaswa kusaidiwa kujenga uwezo ili ziweze kuwahamasisha wananchi kufanya maamuzi kuhusu mustakabali wao.

## Uwekaji wa mifumo na ujenzi wa uwezo wa usimamizi wa mazingira

Hatua mbalimbali za mchakato wa MKUKUTA zilitoa nafasi ya kujifunza na kuweka mifumo ya uandaaji wa vipaumbele vya mazingira.

*Kudumisha maudhui ya sera* – MKUKUTA umesaidia kuendesha mashauriano ya kitaifa kuhusu masuala ya mazingira ambayo yamejenga uwezo katika kuchambua na kujadili masuala muhimu. Changamoto iliyopo hivi sasa ni kuboresha mfumo endelevu wa ushirikishaji ambao utadumisha jitihada hizi na kujenga uwezo wa wadau kuendelea kufanya uchambuzi na majadiliano ya namna hiyo katika ngazi zote.

*Kuendeleza ari na Uratibu* – Programu ya kujumuisha masuala ya mazingira katika MKUKUTA inayoratibiwa na OMR imetoa msukumo mkubwa katika kuboresha usimamizi wa mazingira na kukuza uchumi wa wadau na sekta mbalimbali zinazotekeleza MKUKUTA. Mwamko huu unapaswa kuendelezwa. Juhudi zaidi katika kuratibu ujumuishaji wa masuala mtambuka katika mipango zinahitajika.

*Uimarishaji wa uwezo wa wananchi na asasi za mazingira* – Uimarishaji wa majukumu ya asasi zinazoshughulikia masuala ya mazingira ni muhimu katika kufanikisha matokeo. Baadhi ya asasi za mazingira zimeshaanza kujihusisha na shughuli za kupunguza umaskini. Wako tayari kubadilika, hasa kutokana na ushiriki wao katika mchakato wa MKUKUTA.

Matarajio ya MKUKUTA ni kusaidia jamii iondokane na umaskini. Pia, Sheria ya Mazingira inabainisha majukumu ya wananchi na inazitaka serikali za mitaa na sekta mbalimbali kuteua watendaji mbalimbali watakao simamia matumizi endelevu ya mazingira.

*Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa umaskini na mazingira*

Fursa za kukuza uchumi na kuboresha maisha zinapotea kila mwaka kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kuweka kumbukumbu za maliasili, kwa mfano; upatikanaji wa mazao ya misitu, samaki, wanyamapori na maji. Sheria ya mazingira inazitaka taasisi husika kuanzisha mfumo wa utunzaji wa taarifa za mazingira. Mfumo huu unapaswa kujumuishwa katika Mfumo wa Ufuatiliaji wa Umaskini ambao unahitaji kuwianishwa na mifumo mingine ya ufuatiliaji, kama

vile, (Tahakiki ya Matumizi ya fedha za Umma na Mfumo wa Tathmini ya Utendaji (Perfomance Assesment Framework, PAF). Taarifa ya mwaka ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (Poverty and Human Development, Report) ni mojawapo ya taarifa muhimu zinazoonyesha uwiano wa masuala ya umaskini na mazingira. Orodha ya viashiria vya mazingira inaweza kuwa kiungo katika uandaaji wa taarifa nyingine zinazohitajika kufanya maamuzi ya matumizi endelevu ya rasilimali kwa ajili ya kukuza uchumi. Uandaaji wa mfumo kamilifu ni jambo la muda mrefu, hata hivyo, hauna budi kuandaliwa vizuri. Mfumo wa Milenia wa uandaaji wa tathmini ya mifumo-ikolojia ambao ni mbinu mpya ya kimataifa inayounganisha ubora wa maisha ya watu na mazingira yao kwa kutumia dhana ya manufaa ya mazingira unaweza kuwa mfumo unaokubalika wa utoaji wa taarifa.

*Usimamizi wa mazingira unaojitegemea*

Hivi sasa, asasi za kiraia zimekubalika kuwa wadau muhimu katika kutekeleza majukumu ya serikali kwa kutoa huduma mbalimbali za kijamii na hifadhi ya mazingira. Hata hivyo, ni jambo la muhimu zaidi kwa asasi hizi kuikosoa serikali, hasa katika masuala yanayohitaji mabadiliko kuhusu matumizi ya rasilimali na utawala bora.

*Kukuza uwekezaji katika usimamizi wa mazingira*

Mchakato wa MKUKUTA umechangia katika kufanikisha ongezeko la bajeti katika sekta ya Mazingira. Hata hivyo, mafanikio haya yatakuwa ya kweli iwapo viashiria vya msingi vya sekta nyingine vitaonyesha ongezeko la bajeti na matumizi kwenye shughuli za umaskini na mazingira.



Jambo la muhimu ni kuainisha manufaa yanayotokana na kuongeza fedha katika matumizi ya kuboresha mazingira na ustawi wa jamii. Uboreshaji wa uwezo wa mamlaka za mazingira kuziwezesha kutoa taarifa za msingi za uhakiki wa matumizi ya serikali utakuwa wa manufaa katika kuwezesha utambuzi wa mchango wa maliasili katika kukuza uchumi na kuonyesha umuhimu wa uwekezaji katika utunzaji na uboreshaji wa maliasili hizo.

Mfumo wa ufuatiliaji wa umaskini unabainisha kwamba mpaka sasa kumekuwa na ushirikishaji mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa MKUKUTA, hata hivyo, taarifa sahihi za uwekezaji huo zitahitajika, kwa mfano:

- Mapato halisi yanayotokana na uwekezaji katika maliasili na mazao yake;
- Manufaa yanayopatikana kutokana na kutunza mazingira;
- Mikakati wanayoweza kutumia wawekezaji kuboresha mazingira;
- Uendelezaji wa soko la bidhaa na huduma za mazingira.

Aidha, vyombo vya fedha na washirika wa maendeleo ni wadau muhimu katika kufikia Lengo la Saba la Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambalo kusudio lake ni kuhakikisha kuna uendelevu wa kimazingira. Lengo hili ni mojawapo ya Malengo ya Milenia ambayo yanahitaji misaada ya wafadhili kutokana na utekelezaji wake kutokuwa wa kuridhisha.

# Uzoefu uliotokana na ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika MKUKUTA

Mpaka sasa ni dhahiri kuwa uzoefu wa Tanzania katika ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mchakato wa MKUKUTA umetokana na matukio na sababu mbalimbali. Aidha, kupitia MKUKUTA tumejifunza kuwa ushirikishwaji, ari na utashi ni mambo muhimu katika kufanikisha mipango na mikakati. Haya yote yamesaidia kufanikisha ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo ya asasi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

- Ofisi ya Makamu wa Rais-yenye dhamana ya kushughulikia masuala ya mazingira na umaskini;
- Kikundi cha wataalam wa mazingira ambao walianza kufanya kazi katika miaka ya 1990;
- Programu ya kujumuisha masuala ya mazingira katika waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ilivyoanza mwaka mmoja kabla ya uhakiki mkubwa wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini kufanyika;
- Kuundwa kwa kikundi cha washirika wa maendeleo chenye uwezo mkubwa wa masuala ya mazingira;
- Kukuza ari ya kujitegemea katika kushughulikia mahitaji ya wananchi na fursa mbalimbali zilizopo;
- Tathimini shirikishi ya umaskini ambayo ilieleza bayana kuwa mazingira ni kipaumbele cha kwanza kwa watu maskini; na
- Wizara ya fedha ambayo ilihitajika kuchunguza matumizi na mapato yanayotokana na shughuli za mazingira kama sehemu ya mchakato wa Tahakiki ya Matumizi ya Fedha za Umma.

Hivyo, ujumuishaji wa masuala ya mazingira umefanikishwa na wasimamizi mbalimbali na unahitaji mbinu nyingi. Mafanikio haya yatategemea ushirikiano na ari ya kujumuisha masuala ya mazingira. Aidha tumejifunza kuwa ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango unahitaji utashi wa kisiasa wa serikali ambao hauwezi kufanikishwa kwa kutumia mradi au kikundi cha watu wachache kama wasomi bali kwa kuhusisha wadau wote. Mambo mengine muhimu katika mchakato huu yalikuwa:

*1. Uongozi*

Uongozi ni muhimu katika ujumuishaji wa masuala ya mazingira unaohitaji muda wa kutosha na unafanikishwa na wanaharakati wote wa masuala ya mazingira hasa wazalendo ambao wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja na kuwezeshwa. Washiriki wa nje wanaweza kusaidia kwa kuungana na kushirikiana na wanaharakati kufanikisha utekelezaji.

*2. Mazingira ni kigezo muhimu katika jitihada za kupunguza umaskini*
Mazingira hayapaswi kuonekana kuwa kikwazo cha shughuli za maendeleo. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha kwamba jamii inahusishwa kwa ukamilifu katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na kutafuta mbinu za kuboresha hali ya maisha ya wafugaji, wakulima na makundi mengine; ikiwa ni pamoja na kubadili fikra na mitazamo ya asasi zinazojihusisha na masuala ya mazingira, asasi zisizo za serikali (AZISE) na wengineo, kuwa na msimamo wa matumizi endelevu badala ya ulinzi wa mazingira na kuyaona mazingira kama kichocheo cha maendeleo na msingi wa maisha.

*3. Uwiano kati ya Maendeleo na hifadhi ya Mazingira*
Shughuli za maendeleo zinapaswa kusaidia hifadhi ya mazingira vinategemeana. Hata hivyo, mambo mengine muhimu ni uwezo wa mifumo-ikolojia na mahitaji ya msingi ya ustawi wa jamii ambayo yanayopaswa kulindwa. Pia, majadiliano na taratibu za utoaji wa maamuzi zilizo bayana ni mambo ya muhimu, hata kama hayakubainishwa katika lengo la awali la ujumuishaji wa masuala ya kimazingira.

*4. Kupata uthibitisho na kubadilishana uzoefu*
Kukuza uelewa unaochangia katika kuleta mabadiliko ya fikra na tabia za watu ni jambo la muhimu katika kuonyesha uhusiano kati ya masuala ya umaskini na mazingira. Hata hivyo, uhusiano huo bado haujachambuliwa kwa kina katika nchi nyingi. Hivyo, ipo haja kubwa ya kufanya utafiti, uchambuzi na kubadilishana uzoefu na watoaji maamuzi na umma kwa ujumla. Aidha, taarifa na takwimu sahihi na za kutosha ni muhimu.



*5. Wadau wote wapewe fursa ya kutoa michango yao na kupata mrejesho*
Mitazamo, uelewa na mabadiliko ya utendaji wa sekta na wadau mbalimbali katika masuala ya mazingira yanaweza kusaidia au kuchochea changamoto katika usimamizi. Sekta zina uelewa na tafsiri tofauti ya mazingira. Kutokana na hali hii, wadau wengine hudhani kuwa hawafanyi chochote katika jitihada ya kuhifadhi mazingira, ijapokuwa kwa kweli wanafanya (kwa mfano sekta za maji na afya). Kurekebisha hali hiyo, majadiliano na kuwa na mwongozo wa majukumu ya usimamizi wa mazingira kwa kila sekta itasaidia kurekebisha hali hiyo.

*6. Kuzingatia maoni ya maskini ni muhimili wa kujumuisha masuala ya mazingira na Maendeleo:*
Tofauti na mtazamo wa sekta nyingi, maskini wanajua vyema mazingira yao na uhusiano kati ya umaskini na mazingira. Ushirikishwaji wa watu maskini ili kufahamu fikra na uzoefu wao huharakisha ujumuishaji wa masuala ya mazingira. Mchakato wa ushirikishaji unahitaji muda wa kutosha, fedha na utashi wa kisiasa, lakini unaanzisha na kuendeleza umilikaji wa kweli wa mikakakti na sera zinazofaa. Bila mchakato huo, masuala ya mazingira yatachukuliwa kama kitu kisichokuwa na umuhimu.

*7. Sekta binafsi lazima ishirikishwe katika mchakato:*
Uzoefu wa Tanzania unaonyesha kuwa sekta binafsi haijashirikishwa kwa ukamilifu katika ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika mipango. Sekta hii isiposhiriki kwa ukamilifu itakuwa vigumu sana kuvutia uwekezaji na kuweka motisha kwa ajili ya ubunifu, maendeleo ya teknolojia na mabadiliko ya kifikra. Sekta binafsi ni kichocheo muhimu cha uwekezaji na maendeleo hivyo ipo haja ya kuwashirikisha mapema katika mchakato.

*8. Uwianishaji wa misaada ya wafadhili*
Michango ya wafadhili inapaswa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa. Kwa mfano, kuchangia katika bajeti ya serikali katika masuala ya umaskini na mazingira na kuratibu shughuli na michango ya wafadhili ni muhimu katika utekelezaji wa michakato mingi ya kitaifa. Hivi sasa michakato hiyo inasaidiwa zaidi kwa msaada wa bajeti ya kawaida au mikakati ya misaada ya ushirikiano. Katika uendelezaji wa jitihada hizo, wafadhili hawana budi kushughulikia kwa ukamilifu masuala ya mazingira - hasa kwa kuzingatia uhusiano wa umaskini na mazingira ili kuboresha mashauriano ya kisera kati ya wafadhili na serikali.

*9. Misaada izingatie mahitaji:*
Misaada ya kiufundi ya kujumuisha masuala ya mazingira lazima izingatie mahitaji na matakwa ya wadau hususan wananchi na ipatikane katika muda unaofaa. Kama misaada hiyo itatolewa, basi iwe ni ile isiyopatikana nchini na ilenge katika kujenga uwezo wa wataalamu wazalendo na wananchi.



*10. Umuhimu wa Bajeti*
Ushirikishwaji wa sekta katika kujumuisha masuala ya mazingira utafanikiwa kwa kuhakikisha kuwa wizara za kisekta zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya hifadhi ya mazingira. Viashiria vya mafanikio ya ujumuishaji wa masuala ya mazingira ni kujumuishwa katika mchakato wa bajeti, wa kila sekta (ikiwa ni pamoja na serikali kuu na taasisi zake) na katika mifumo ya ufuatiliaji wa matumizi.

*11. Ushirikiano wa wadau wanaoshughulikia masuala mtambuk*a
Mazingira siyo suala pekee mtambuka ambalo halikupewa umuhimu unaostahili katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini na michakato mingine ya upangaji mipango ya kitaifa. Masuala ya jinsia na UKIMWI pia yamepata changamoto katika ujumuishaji huo. Matokeo ya kuunganisha makundi mbalimbali mtambuka wakati wa michakato ya sera ni pamoja na (i) kuyawezesha makundi hayo kubadilishana uzoefu na utendaji; (ii) kuboresha ushirikiano kati ya makundi hayo, na (iii) kupunguza gharama za majadiliano na kila kundi.

*12. Umuhimu wa kuendesha mchakato wa ujumuishaji kwa muda muafaka*
Ujumuishaji wa masuala ya mazingira na masuala mengine mtambuka unapaswa kufanywa mwanzoni mwa mchakato. Itakuwa bora zaidi kuainisha kwanza mambo muhimu hasa yale ambayo ni mtambuka na kisha kutafuta jinsi ya kuyajumuisha

mwanzoni mwa michakato na katika uhakiki wa shughuli mpya. Utendaji wa namna hiyo utawezesha masuala hayo kupewa umuhimu unaostahili, kuwa na utaratibu wa mustakabali wa ujumuishaji, na matumizi bora ya fursa zilizopo.

## Hitimisho:

MKUKUTA umekuwa nyenzo muhimu katika kuweka mtazamo mpya wa kuwahusisha wadau katika maamuzi ya sera juu ya matumizi na uendelezaji wa rasilimali katika kuendesha maisha yao. MKUKUTA umeanzisha utaratibu unaothamini ushirikishwaji wa wadau katika upangaji wa Mipango. Aidha, umeanzisha utaratibu mpya unaokubalika ambao ni shirikishi zaidi katika jitihada za kupunguza umaskini na kuhifadhi mazingira. Utaratibu huu utawezesha wadau wengi zaidi kujadili mikakati ya maendeleo ya Tanzania, na umeimarisha ushirikiano kati ya watoa maamuzi kama vile Wizara ya Fedha na Mipango na sekta nyingine ambazo hutoa huduma kwa wananchi. Tunashukuru kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na mchakato wa kujumuisha masuala ya mazingira katika MKUKUTA.

# Rejea

Bojo, J. and R.C. Reddy. 2003. Status and evolution of environmental priorities in the Poverty Reduction Strategies: A review of 50 Poverty Reduction Strategy Papers. World Bank Environmental Economics Series paper no. 93.

Economic and Social Research Foundation. 2003. Vulnerability and resilience to poverty in Tanzania: summary of the 2002/3 Tanzania Participatory Poverty Assessment.

Geoghegan, T. 2007 (forthcoming). Making aid work better for recipients – and improving national planning processes for sustainable development in the bargain. IIED Sustainable Development Opinion Paper.

Vice-President's Office, United Republic of Tanzania. 2005. National Strategy for Growth and Reduction of Poverty.

Vice-President's Office, United Republic of Tanzania. 2004. Public Expenditure Review of Environment Financial Year 2004.

Vice-President's Office, United Republic of Tanzania. 2004a. Guide and Action Plan to mainstreaming environment into the Poverty Reduction Strategy review.

Waldman, L. 2005. Environment, politics and poverty: lessons from a review of PRSP stakeholder perspectives. Institute of Development Studies, Brighton.

World Bank. 2005. Study on growth and environment links for preparation of the Country Economic Memorandum (CEM).

## Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Tanzania

Watu maskini wanategemea kwa kiwango kikubwa Mazingira na rasilimali zake kama maji safi na ardhi yenye rutuba. Aidha, wao ni wahanga wakubwa wa majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira. Hali kadhalika ukuaji wa uchumi pia hutegemea maliasili na mazingira. Hivyo ni muhimu kujumuisha masuala ya Mazingira katika mchakato wa Mipango na maendeleo. Tathmini ya awali inaonesha suala la Mazingira halijapewa kipaumbele katika mikakati mingi ya kupambana na umaskini inayoandaliwa na nchi mbalimbali. Je ukweli ni upi, na lipi laweza kufanyika juu ya jambo hili?

Waandishi wa Kitabu hiki wameonesha jinsi Tanzania ilivyoweza kufanikisha jambo hili, wadau, juhudi mbali mbali zilizofanyika, matukio na uzoefu uliopatikana katika kujumuisha Masuala ya Mazingira katika mchakato wa kupambana na Umaskini. Mafanikio mengi yametokana na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) ambao uliwezesha kujumuisha masuala ya Mazingira. Waandishi wameelezea kwa undani mchakato huu,mafanikio yake, changamoto na kutoa mwongozo kwa nchi nyingine zinazokusudia kujifunza.

Kitabu hiki kimetolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania.

**Toleo la Maliasili Na. 6**

ISBN: 978-1-84369-723-7
ISSN: 1605-1017

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

iied

International Institute for Environment and Development